## Idara ya Elimu Sekondari

Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe ina Jumla ya Shule za Sekondari 17, kati ya hizo 14 ni za serikali, shule tatu (3) za binafsi. Shule hizi zina jumla ya wanafunzi 10,482 wavulana 5,778 na wasichana 4,704. Huduma mbalimbali za elimu ya sekondari zimekuwa zikiboreshwa zaidi kama inavyoonekana katika majedwali hapa chini.

### Idadi ya shule za sekondari na walimu

| **Wilaya** | **Serikali** | **Binafsi** | **Jumla** | **Idadi ya walimu** | | | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | **Mahitaji** | **Waliopo** | | |
| | | | | | **ME** | **KE** | |
| Bukombe | 14 | 3 | 17 | 651 | 358 | 163 | 521 |

Kutokana na takwimu za walimu kwenye jedwali hapo juu, Halmashauri ina upungufu wa walimu 168 wa sayansi. Kwa mwaka 2015 halmashauri ya wilaya ya Bukombe ilipangiwa jumla ya walimu wa sayansi na sanaa mia nne tisini na mbili (492). Stashahada 180, na Shahada 312, walioripoti walikuwa 438, sawa na 89% kama ilivyo katika jedwali.

### Mwenendo wa kuripoti walimu 2017/18

| Walimu wa Stashahada | | | | Walimu wenye Shahada | | | | Jumla | | Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Waliopangwa | Walioripoti | | | Waliopangwa | Walioripoti | | | Pangwa | Ripoti | |
| | Sanaa | Sayansi | Jumla | | Sanaa | Sayansi | Jumla | | | 100 |
| 15 | 0 | 10 | 10 | 5 | 0 | 5 | 5 | 15 | 15 | |

Tunaishukuru serikali kwa kuendelea kutoa ajira kwa walimu wa masomo ya sayansi. Kwani kuongezeka kwa walimu hawa kutaboresha ufundishaji wa masomo ya sayansi hivyo kuinua kiwango cha elimu nchini na kufikia malengo ya Tanzania ya Viwanda.

### Mahudhurio ya wanafunzi

Hali ya mahudhurio kwa wanafunzi wote kidato cha I-VI ni ya kuridhisha, asilimia ya mahudhurio hadi juni 2018 ilikuwa 86.%. Hata hivyo kumekuwa na tatizo la watoto wa kike

kupata ujauzito wakiwa shuleni, tangu Julai 2017 hadi Juni 2018 wanafunzi wa kike 39 walipata mimba. Mchanganuo wake umeonyeshwa kataka jedwali lifuatalo:-

## Mimba shuleni

| Mwaka | Idadi ya wanafunzi wa kike | Idadi ya waliopata mimba | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 2017 | 3,538 | 28 | 0.7 |
| 2018 | 4,624 | 11 | 0.2 |

Uongozi wa Halmashauri umechukua hatua mbalimbali kupunguza tatizo hili ikiwa pamoja na

- Kamati za ushauri shuleni kutoa elimu ya uzazi kwa wanafunzi
- Kuimarisha mikakati ya ujenzi wa Hosteli za wasichana katika shule za sekondari hadi sasa Hosteli za Namonge na Ushirombo zinatumika.
- Kesi za mimba zimefikishwa katika vyombo vya sheria kwa maamuzi.

## Miundombinu ya elimu sekondari

## Ujenzi wa majengo shule za sekondari

| Aina ya Majengo | Mahitaji | Vyumba vilipo hadi Juni 2018 | Majengo Hatua za Msingi | Hatua ya renta, Maboma | Hatua ya Kupauliwa | Majengo Yaliyopo hatua ya ukamilishaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Madarasa | 286 | 131 | 5 | 15 | 4 | 2 |
| Matundu yaVyoo vya Wanafunzi | 420 | 178 | 24 | 0 | 0 | 0 |
| Matundu ya Vyoo vya Walimu | 56 | 56 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Majengo ya Utawala | 14 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Nyumba za Walimu | 494 | 59 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Vyumba vya Maabara | 42 | 32 | 0 | 1 | 0 | 09 |

- Vyumba 32 Vya maabara vimekamilika na vinatumika (vikiwa na samani zake).

- Hivyo Vyumba 09 vipo katika hatua ya ukamilishaji.
- Chumba 01 kipo hatua ya boma.

## Changamoto

- Upungufu wa walimu wa sayansi 168
- Upungufu wa vyumba vyumba vya madarasa 155
- Upungufu wa nyumba za walimu 435
- Uhaba wa Vifaa vya Maabara kati ya shule 14 ni shule 5 tu zina vifaa vya maabara vinavyotosheleza

## Mikakati

Halmashauri kwa kushirikiana na Serikali kuu na wadau mbalimbali wa elimu itaendelea kutatua changamoto zilizopo kama ifuatavyo:-

(i) Halmashauri kuendelea kutenga bajeti ya ujenzi wa madarasa na nyumba za walimu kwa kila shule ili kukabiliana na upungufu uliopo.

(ii) Kuendelea kuiomba serikali kuajiri walimu wa sayansi ili kukabiliana na upungufu wa walimu wa sayansi.

(iii) Kuendelea kuhamasisha jamii ya kila shule kujenga na kukamilisha miundombinu ya shule husika.

## Kazi za Idara

- Kumshauri Mkurugenzi wa Halmashauri kuhusu shughuli zote zinazohusu Idara ya Elimu ya Sekondari
- Kusimamia mitihani yote ya ndani na ile ya Taifa yaani Mitihani ya kidato cha II, IV na VI.
- Kusimamia, kuratibu na kufuatilia shughuli za ujenzi wa miundombinu katika shule za Sekondari kama vile nyumba za walimu, madarasa, majengo ya utawala, maabara, mkataba na vyoo
- Kusimamia na kuratibu shughuli zote za ukusanyaji, uchambuzi na kutafsiri takwimu za idara ya elimu sekondari na kuzituma kwa wadau wa elimu
- Kusimamia na kuratibu shughuli za uandaaji wa taarifa na kuzituma kwa wadau mbalimbali wa elimu ngazi ya Wilaya, Mkoa na Taifa
- Kusimamia na kuhakikisha kuwa wanafunzi wanapata taaluma kwa kiwango kilicho bora kwa mujibu wa Sera ya Elimu ya mwaka 1995 na 2014.
- Kusimamia na kuhakikisha nidhamu ya wanafunzi, walimu na watumishi wasio walimu inadumishwa shuleni

- Kusimamia na kuhakikisha fedha za Idara ya Elimu Sekondari zinatumika kwa kufuata kanuni, sheria, taratibu na miongozo ya fedha za Serekali za Mitaa
- Kuhakikisha vifaa vya kufundishia na kujifunzia vinapatikana katika shule za sekondari
- Kuhakikisha kuwa shule zote za Sekondari zina samani za kutosha kwa ajili ya walimu na wanafunzi
- Kuandaa ajenda na kuhudhuria vikao vyote vinavyohusu Idara ya Elimu Sekondari
- Kuandaa taarifa za utekelezaji za Idara ya elimu sekondari za robo na mwaka na kuziwasilisha kwa wadau mbalimbali wa maendeleo kama vile Waheshimiwa Madiwani, Mkoa na Taifa
- Kuandaa makisio ya bajeti ya Idara ya Elimu ya Sekondari kila mwaka.
- Kupokea na kuwapangia vituo walimu na wafanyakazi wa idara wanaohamia au wanaoajiriwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe.